TANZANIA HIGHER LEARNING INSTITUTIONS TRADE UNION
P.O. BOX **35928 DAR ES SALAAM, Tanzania**
Tel: **022 2401581**, Fax: **022 2401582**
Website: www.thtu.or.tz, Email: thtuhq@gmail.com

# UHURU WA TAALUMA VYUO VIKUU TANZANIA: UCHAMBUZI WA MFUMO WA KISHERIA NA ATHARI ZA UKAMATAJI WA WANATAALUMA

## 1. Utangulizi

Uhuru wa taaluma ni moja ya nguzo muhimu za elimu ya juu na maendeleo ya jamii inayozingatia maarifa, utafiti na ubunifu. Dhana hii inahusu haki ya wanataaluma, watafiti na wanafunzi kufundisha, kujifunza, kufanya utafiti, kuchapisha matokeo ya tafiti na kushiriki katika mijadala ya kitaaluma bila kuingiliwa, kutishwa au kuwekewa vikwazo visivyo halali. Uhuru huo huwezesha vyuo vikuu kutekeleza jukumu lake la msingi la kuzalisha maarifa mapya, kukuza fikra huru, kuchochea ubunifu na kutoa suluhisho la changamoto za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kwa sababu hiyo, uhuru wa taaluma unatambuliwa kimataifa kama moja ya viashiria muhimu vya ubora wa elimu ya juu, maendeleo ya sayansi na uimara wa utawala wa sheria.

Katika miezi ya karibuni, mjadala kuhusu uhuru wa taaluma nchini Tanzania umeongezeka kufuatia matukio ya baadhi ya wanataaluma kutoka vyuo vikuu kukamatwa, kuhojiwa au kufunguliwa mashitaka kwa tuhuma zinazohusiana na maoni au kauli walizotoa wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kitaaluma. Kwa mujibu wa taarifa za Jeshi la Polisi, baadhi ya wanataaluma hao walituhumiwa kwa kufundisha maudhui yanayochochea maandamano. Matukio hayo ya ukamataji yamezua mjadala mpana kuhusu mipaka ya uhuru wa taaluma na namna ambavyo utekelezaji wa sheria unapaswa kuendana na ulinzi wa haki za msingi za wanataaluma.

Kutokana na hali hiyo, kuna umuhimu wa kutathmini iwapo mfumo wa kisheria wa Tanzania unatoa ulinzi wa kutosha kwa uhuru wa taaluma kwa kuzingatia viwango vya kimataifa, kikanda na kitaifa. Andiko hili linachambua dhana na historia ya uhuru wa taaluma, mfumo wa kisheria unaoulinda uhuru huo katika ngazi ya kimataifa, Afrika,

Afrika Mashariki na Tanzania, pamoja na nafasi ya Azimio la Dar es Salaam (Dar es Salaam Declaration), Azimio la Kampala kuhusu Uhuru wa Kitaaluma na Wajibu wa Kijamii (The Kampala Declaration on Intellectual Freedom and Social Responsibility), Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (2019) katika maendeleo ya uhuru wa taaluma. Aidha, andiko linachambua athari zinazoweza kujitokeza kutokana na ukamataji wa wanataaluma kwa mazingira ya elimu ya juu na kutoa mapendekezo ya kisheria na kisera yanayoweza kuimarisha ulinzi wa uhuru wa taaluma nchini.

## 2. Dhana ya Uhuru wa Taaluma

### a. Kwa mujibu wa nyaraka na vyombo mbalimbali

Uhuru wa taaluma ni haki na nafasi inayotolewa kwa wanataaluma, watafiti, wanafunzi na taasisi za elimu ya juu kutafuta, kuzalisha, kuchambua, kuhifadhi, kufundisha na kusambaza maarifa bila kuingiliwa, kutishwa, au kuadhibiwa kwa sababu ya matokeo ya shughuli halali za kitaaluma. Uhuru huu unakusudia kuweka mazingira ambayo ukweli unaweza kutafutwa kwa kutumia mbinu za kisayansi na kitaaluma, hata pale ambapo matokeo, hoja au maoni yanayotolewa hayapendwi na Serikali, uongozi wa chuo, wafadhili, taasisi za dini, makundi ya kisiasa au sehemu fulani ya jamii.[1]

Kwa mujibu wa Pendekezo la Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni kuhusu Hadhi ya Wafanyakazi Wanataaluma katika Elimu ya Juu (UNESCO Recommendation concerning the Status of Higher-Education Teaching Personnel (1997) uhuru wa taaluma unahusisha uhuru wa kufundisha na kujadili bila kufungwa na mafundisho yaliyowekwa;[2] kufanya utafiti na kusambaza au kuchapisha matokeo yake; kutoa maoni kuhusu taasisi au mfumo ambamo mwanataaluma anafanya kazi; kutokabiliwa na udhibiti wa taasisi; na kushiriki katika vyama na vyombo vya kitaaluma. UNESCO inaunganisha uhuru huo na uhuru wa taasisi, ushiriki katika utawala wa chuo, usalama wa ajira na wajibu wa kitaaluma.

[1] Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni, *Maoni ya Jumla Na. 13 kuhusu Haki ya Elimu*, Hati ya Umoja wa Mataifa Na. E/C.12/1999/10, 8 Desemba 1999, aya za 38–40.

[2] Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO). *Pendekezo kuhusu Hadhi ya Wafanyakazi wa Ualimu wa Elimu ya Juu*. Paris: UNESCO, 1997.

Kwa hiyo, uhuru wa taaluma hauishii katika uhuru wa mhadhiri kuzungumza darasani. Ni dhana pana inayohusu mchakato mzima wa maarifa, kuanzia uchaguzi wa jambo la kuchunguza, ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa, uundaji wa hoja, ufundishaji, uchapishaji wa matokeo ya tafiti, mijadala ya kitaaluma, ukosoaji wa taasisi na ushiriki katika uongozi wa masuala ya kitaaluma.

## b. Uhuru wa Taaluma na wa kitaasisi kutoka kwa wanafalsafa na pia Kauli Maarufu (Popular saying)

Wanafalsafa mbalimbali wamejaribu kuelezea maana na mapana ya uhuru wa taaluma kwa namna mbalimbali. Pia zipo kauli maarufu ambazo huwa zinatumika kuelezea dhana ya uhuru wa taaluma na wa kitaasisi. Zifuatazo ni nukuu za baadhi ya wanafalsafa pamoja na kauli maarufu (popular saying) kuhusu uhuru wa taaluma na wa kitaasisi.

Jedwali la Nukuu za Uhuru wa Taaluma

| Na. | Nukuu (Kiswahili) | Quote (English) | Chanzo/Mwanafalsafa |
|---|---|---|---|
| 1 | "Chuo kikuu ambacho hakiruhusu mawazo huru kukua, na ambacho kinajenga hofu badala ya ujasiri wa kuhoji, kinapoteza maana yake ya kuwepo." | "A university which does not allow free ideas to grow, and which builds fear instead of the courage to question, loses its meaning of existence." | Kauli maarufu |
| 2 | "Kwa 'uhuru wa taaluma' ninaelewa haki ya kutafuta ukweli, na kuchapisha na kufundisha kile mtu anachoamini kuwa ni kweli." | "By 'academic freedom' I understand the right to search for truth, and to publish and teach what one holds to be true." | Albert Einstein |
| 3 | "Vyuo vikuu vinapaswa kuwa mahali ambapo mawazo mapya yanazaliwa, ambapo maoni tofauti | "Universities should be places where new ideas are born, where different opinions clash without fear..." | Kauli maarufu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | yanakabiliana bila woga..." | | |
| 4 | "Tunataka vyuo vikuu vyetu viwe vituo vya ubunifu na fikra huru. Uhuru wa kitaaluma ni lazima ulindwe..." | "We want our universities to be centres of creativity and free thought. Academic freedom must be protected..." | Kauli maarufu |
| 5 | "Uhuru wa taaluma si haki ya kipekee ya wasomi; ni haki ya jamii nzima kujua kwamba wanafunzi na walimu wao wana uhuru wa kufikiri..." | "Academic freedom is not a special privilege of academics; it is the right of the whole society to know that their students and teachers are free to think..." | Kauli maarufu |
| 6 | "...uhuru wa wanataaluma wote kutafuta, kukuza, na kusambaza maarifa kupitia utafiti, ufundishaji, na majadiliano bila kuzuiliwa..." | "...the freedom of all academics to pursue, develop, and transmit knowledge through research, teaching, and discussion without restriction..." | Tamko la Lima (1988) |
| 7 | "Uhuru wa kitaaluma si sawa na uhuru wa kujieleza. ... Kukana uhuru katika elimu ni uhalifu dhidi ya demokrasia." | "Academic freedom is not the same as freedom of speech. ... to deny freedom in education is a crime against democracy." | John Dewey |

Jedwali hapo juu, linaonyesha nukuu mbalimbali za watu wenye ushawishi mkubwa (wanafalsafa) katika jamii walio toa mitazamo yao kuhusu uhuru wa taaluma na pia kauli maarufu duniani kuhusu mada tajwa.

## 3. Historia ya Uhuru wa Taaluma

Asili ya uhuru wa taaluma ilianzia katika vyuo vikuu vya Ulaya, hususan katika Chuo Kikuu cha Bologna na Chuo Kikuu cha Humboldt nchini Ujerumani. Mfumo wa Humboldt uliweka msingi wa dhana kwamba ufundishaji na utafiti vinapaswa kufanywa kwa uhuru bila shinikizo kutoka kwa serikali, dini au makundi yenye maslahi binafsi.

Baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, umuhimu wa uhuru wa taaluma ulitambuliwa kimataifa kupitia maendeleo ya haki za binadamu. Mataifa mengi yaliweka mifumo ya kikatiba na kisheria inayolinda uhuru wa kujieleza, uhuru wa kufikiri na uhuru wa kufanya utafiti wa kisayansi. Afrika nayo ilianza kuingiza dhana hii katika sera za elimu ya juu baada ya kupata uhuru, ingawa changamoto za kisiasa na kiutawala zimeendelea kuathiri utekelezaji wake.

Katika ngazi ya taasisi za vyuo vikuu, dhana ya uhuru wa taaluma imetiliwa maanani katika hati idhini za vyuo husika ambazo zimesisitiza kuheshimu uhuru wa taaluma, kwa mfano, hati idhini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inatambua uhuru wa wanataaluma wa kufundisha, kutafiti, kupokea, kubadilishana na kusambaza maarifa bila hofu ya kuingiliwa, kubaguliwa, kuonewa au kukandamizwa.[3]

## 4. Mfumo wa Kisheria wa Uhuru wa Taaluma

Mfumo wa kisheria wa uhuru wa taaluma unatambulika Kimataifa, Barani Afrika, Afrika Mashariki na Tanzania.

### 4.1 Ngazi ya Kimataifa

Kimataifa, uhuru wa taaluma unatambuliwa kupitia vyombo mbalimbali vya haki za binadamu. Ibara ya 19 ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu (Universal Declaration of Human Rights, 1948)*,* linatambua uhuru wa kutoa maoni na kujieleza.[4] Aidha, Ibara ya 19 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (International

[3] Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *Hati Idhini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ya Mwaka 2007*, Tangazo la Serikali Na. 259A la 2007, Ibara ya 4 – Kanuni ya 58(1).

[4] Umoja wa Mataifa, Baraza Kuu, *Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu*, Azimio la Baraza Kuu Na. 217 A (III), lililopitishwa na kutangazwa Paris, Ufaransa, tarehe 10 Desemba 1948.

Covenant on Civil and Political Rights,1966) kinahakikisha haki ya kutafuta, kupokea na kusambaza taarifa na mawazo.[5]

Vilevile, Pendekezo la UNESCO la Mwaka 1997 linatambua uhuru wa wanataaluma wa kufundisha, kufanya utafiti, kuchapisha matokeo ya tafiti na kushiriki katika mijadala ya kitaaluma bila hofu ya vitisho, ubaguzi au adhabu isiyo halali.[6]

### 4.2 Afrika

Katika Afrika, msingi wa kisheria wa uhuru wa taaluma unatokana na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981 (African Charter on Human and Peoples Rights, 1981) hususan Ibara ya 9 inayolinda uhuru wa kujieleza na Ibara ya ya 17 inayotambua haki ya elimu. Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu imefafanua uhuru wa taaluma kama sehemu ya haki ya uhuru wa kujieleza na maendeleo ya jamii zinazoheshimu misingi ya kidemokrasia.[7]

### 4.3 Afrika Mashariki

Katika ngazi ya Afrika Mashariki, Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki unahimiza ushirikiano katika masuala ya elimu ya juu, sayansi na teknolojia pamoja na kuheshimu haki za binadamu, utawala bora na utawala wa sheria.

Aidha, mwaka 1990 Azimio la Kampala (Kampala Declaration on Intellectual Freedom and Social Responsibility)[8] kuhusu Uhuru wa Kitaaluma na Wajibu wa Kijamii, lililopitishwa mjini Kampala, Uganda na Baraza la Maendeleo ya Utafiti wa Sayansi ya Jamii Barani Afrika (CODESRIA), liliweka msingi muhimu wa kulinda uhuru wa wanataaluma katika ukanda wa Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla.[9] Tamko hili linasisitiza kuwa:

---

[5] Umoja wa Mataifa, Baraza Kuu, *Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa*, Azimio la Baraza Kuu Na. 2200 A (XXI), Hati ya Umoja wa Mataifa Na. A/RES/2200A(XXI), uliopitishwa New York tarehe 16 Desemba 1966 na kuanza kutumika tarehe 23 Machi 1976, United Nations Treaty Series, Juzuu ya 999

[6] Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO). *Pendekezo kuhusu Hadhi ya Wafanyakazi wa Ualimu wa Elimu ya Juu*. Paris: UNESCO, 1997.

[7] Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU), *Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu*, Hati ya OAU Na. CAB/LEG/67/3 Rev. 5, 27 Juni 1981, Ibara ya 9.

[8] Ibara ya 3 ya Azimio la Kampala kuhusu Uhuru wa Kiakili na Wajibu wa Kijamii, 1990.

[9] Ibid, 1990

i. Uhuru wa kufikiri, kufanya utafiti na kusambaza maarifa ni haki ya msingi ya kila msomi;
ii. Serikali zina wajibu wa kuhakikisha mazingira salama ya kufanya tafiti na kushiriki katika mijadala ya kitaaluma;
iii. Vyuo vikuu vinapaswa kuwa na uhuru wa kujiendesha (Institutional Autonomy) bila kuingiliwa na mamlaka za kisiasa;
iv. Wanataaluma wanapaswa kutumia uhuru wao kwa uadilifu, uwajibikaji na kuzingatia maadili ya taaluma.

Kwa kufanya hivyo, Azimio la Kampala limekuwa rejea muhimu katika kuimarisha uhuru wa taaluma katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki.

### 4.4 Tanzania

Nchini Tanzania, msingi wa kisheria wa uhuru wa taaluma unatokana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, hususan ibara ya 18 inayolinda uhuru wa kutoa maoni, kujieleza na kupata taarifa.[10] Aidha, Sheria ya Vyuo Vikuu, 2005 inatambua uhuru wa taasisi za elimu ya juu.[11]

Mwongozo wa Viwango na Miongozo ya Elimu ya Vyuo Vikuu nchini (Handbook for Standards and Guidelines for University Education in Tanzania), Toleo la Tatu unaitaka TCU kukuza uhuru wa kitaaluma.

Mbali na mfumo huo wa kisheria, Tanzania imechangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya uhuru wa taaluma kupitia Azimio la Dar es Salaaam (Dar es Salaam Declaration on Academic Freedom and Social Responsibility of Academics, 1990). Tamko hili lilipitishwa tarehe 19 Aprili 1990 jijini Dar es Salaam na limekuwa moja ya nyaraka muhimu zaidi kuhusu uhuru wa taaluma barani Afrika.

Azimio la Dar es Salaam linasisitiza kwamba:

i. Elimu ni haki ya msingi ya binadamu na nyenzo ya maendeleo ya jamii;[12]

---

[10] Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977,
[11] Sheria ya Vyuo Vikuu, Sura ya 346, Toleo la 2023.
[12] Ibara ya 3 ya Dar es Salaam Declaration on Academic Freedom and Social Responsibility of Academics, 1990.

ii. Vyuo vikuu vinapaswa kuwa huru dhidi ya uingiliaji wa kisiasa au maslahi binafsi;[13]
iii. Wanataaluma wana haki ya kufundisha, kufanya utafiti, kuchapisha matokeo ya tafiti na kutoa maoni ya kitaaluma bila hofu ya vitisho au adhabu;[14]
iv. Uhuru wa taaluma unapaswa kuambatana na uwajibikaji wa kijamii na maadili ya taaluma;
v. Wanafunzi wanapaswa kuwa na uhuru wa kujifunza na kushiriki katika mijadala ya kitaaluma bila ubaguzi au kunyanyaswa.

## 5. Ukamatwaji wa Wanataaluma

Mnamo tarehe 3 Julai 2026, wahadhiri wawili wa Chuo Kikuu cha ***St. John*** cha Tanzania (SJUT)[15] **ambao pia ni wanachama hai wa THTU** walikamatwa wakiwa katika maeneo yao ya kazi wakitekeleza majukumu yao. Kwa mujibu wa taarifa zilizopo, wahadhiri hao walikamatwa kwa sababu mbili tofauti (kila mmoja na sababu yake). Mmoja alikamatwa kutokana na maudhui ya mada inayohusiana na *Maadili na Utawala bora* aliyofundisha darasani siku ya Jumanne tarehe 31/06/2026. Tulielezwa kwamba, wakati anafundisha, alitoa mifano ya kashfa mbalimbali zilizowahi kutokea hapa Tanzania mfano Richmond, ESCROW na nyingine na namna wanasiasa walivyowajibika kwa kutozingatia taratibu. Lengo la mifano hiyo kwa mujibu wa mhusika ni kuwaelewesha wanafunzi umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu wanapotekeleza majukumu yao baadae watakapokuwa kazini. Mhadhiri wa pili ambae pia ni Mkurugenzi wa Huduma za Wanafunzi yeye ukamataji wake unahusishwa na masuala ya uchaguzi wa wanafunzi wa chuo hicho. Wote wawili walikamatwa kwa tuhuma za kuhamasisha maandamano ya tarehe 07.07.2026. Kukamatwa kwao wakiwa katikati ya utekelezaji wa majukumu yao ya kazi kumeibua maswali kuhusu namna Jeshi la Polisi linavyoingilia uhuru wa taaluma.

[13] Ibara ya 20 ya Dar es Salaam Declaration on Academic Freedom and Social Responsibility ofAcademics, 1990.
[14] Ibara ya 14 ya Dar es Salaam Declaration on Academic Freedom and Social Responsibility of Academics, 1990.
[15] Wahadhiri waliokamatwa ni Johaiven Revelian Bikongolo na Titus Joseph Kituli wa Chuo Kikuu cha St John cha Tanzania

Ukamataji huu ulikiuka misingi ya kisheria kwa **kutokuwapa waajiri wao taarifa** za kukamatwa kwao na bila kuwapatia wahadhiri hao haki zao za msingi kama zinavyotambuliwa na sheria, ikiwemo **haki ya kujulishwa makosa wanayotuhumiwa kufanya na haki ya kuwajulisha ndugu**, **jamaa au marafiki kuhusu kukamatwa kwao**.

Mhadhiri mwingine wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)[16] nae alikamatwa baada ya kuitikia wito wa Jeshi la Polisi iliyomtaka afike kituo kimojawapo cha Polisi kwa tuhuma hizo hizo za maandamano. Bahati mbaya zaidi, huyu wa UDOM ni mara ya pili anakamatwa baada ya mara ya kwanza kukamatwa mwaka jana kwenye vuguvugu la maandamano ya tarehe 09.12.2025.

Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU) kimefuatilia suala hili katika Kituo cha Polisi Chang'ombe ambapo wahadhiri hao wanashikiliwa. THTU ilifika pia katika Ofisi za Polisi Mkoa wa Dodoma, kwa lengo la kuhakikisha wanapata haki yao ya msingi ya dhamana. Hata hivyo, juhudi hizo hazikuzaa matunda, kwani Jeshi la Polisi limeendelea kuwanyima dhamana kwa msisitizo kwamba suala hilo linahusu **ulinzi na usalama wa nchi**. Wahadhiri hao wamekuwa wakishikiliwa na jeshi hilo kuanzia walipokamatwa **tarehe 3 Julai 2026** mpaka tunapokamilisha andiko hili **tarehe 20 Julai, 2026**.

Ifahamike wazi kwamba haki ya kupata dhamana ni miongoni mwa haki za msingi za mtuhumiwa, kama inavyotambuliwa na kulindwa chini ya Ibara ya 13(6)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inayoweka msingi wa dhana ya kutokuwa na hatia hadi pale mahakama itakapothibitisha hatia[17]. Aidha, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inaainisha kwa uwazi makosa yanayostahili dhamana na yale yasiyostahili dhamana.[18]

Wahadhiri hao wanakabiliwa na tuhuma za **kosa la uchochezi, ambalo kwa mujibu wa sheria ni kosa linalostahili dhamana**. Hivyo, kuendelea kuwashikilia

---

[16] Mhadhiri wa UDOM aliyekamatwa ni Melkisedeki Kitunzi Kaijage

[17] Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 13(6)(b) na Ibara ya 15(1)–(2).

[18] Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, Toleo la 2023, kifungu cha 151(1)–(7).

bila kuwapatia dhamana, bila kuwepo msingi wa kisheria unaoruhusu hatua hiyo, kunazua maswali kuhusu uzingatiaji wa Katiba, utekelezaji wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, na ulinzi wa haki za msingi za watuhumiwa. Pamoja na kulaani kitendo hiki, THTU inaendelea kufuatilia upatikanaji wa dhamana kwa watuhumiwa mpaka watakapopata haki hiyo ambayo walipaswa kupatiwa toka walivyokamatwa.

**Vilevile, ni haki ya kila mtuhumiwa anayekamatwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kutenda kosa la jinai kufikishwa mahakamani ndani ya saa 24 ili ajibu tuhuma zinazomkabili, kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo, kitendo cha Jeshi la Polisi kuwashikilia wahadhiri hao kwa muda wa siku 17 bila kuwafikisha mahakamani ni kinyume na matakwa ya sheria na kinatafsirika kama kuwanyima uhuru wao isivyo halali.**

Pia, THTU itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha kwamba maboresho na mabadiliko mbalimbali yanafanyika kama inavyoelezwa kwenye mapendekezo ya andiko hili kwa ajili ya sasa na baadae.

## 6. Athari za Ukamataji wa aina hii

Kukamatwa kwa wanataaluma kuna athari nyingi kwa mtu binafsi na familia (mtuhumiwa), athari kwa serikali na pia athari kwa taaluma. Kwa upande wa mtu binafsi, ukamataji wa aina hii unaleta athari kubwa kisaikolojia, kihisia na kimwili huku familia ikiingia kwenye usumbufu mkubwa na gharama za kumfuatilia mpendwa wao. Kutokana na hili, Serikali inaingia kwenye lawama kubwa kwamba haijali watu wake na zaidi sana Katiba na Sheria hazizingatiwi. Ukiachana na hizi athari za moja kwa moja kwa mhusika na familia, zipo athari mbalimbali kwa upande wa taaluma kama inavyoelezwa hapa chini:-

Kwanza, **ukamataji unazalisha hofu (chilling effect) vyuo vikuu**. Uhuru wa taaluma unategemea uwezo wa wanataaluma kufundisha, kufanya utafiti na kushiriki katika mijadala ya kitaaluma bila hofu ya kulengwa kwa sababu ya mawazo wanayotoa katika muktadha wa taaluma. Pale ambapo wanataaluma wanashuhudia wenzao wakikamatwa kuhusiana na maudhui ya mihadhara, mijadala au ushiriki wao katika masuala ya umma, kuna uwezekano wa kuanza kujizuia kujadili mada zinazoweza

kuonekana kuwa nyeti. Hali hii husababisha *self-censorship*, ambapo mwalimu au mtafiti huchagua kutofundisha au kutafiti masuala fulani kwa kuhofia madhara ya kisheria au kiutawala.

Pili, **ukamataji wa wanataaluma unaathiri ubora wa ufundishaji vyuoni**. Elimu ya chuo kikuu haikusudii kutoa maarifa ya kinadharia pekee bali kuwajengea wanafunzi uwezo wa kuchambua hoja, kuhoji mawazo yaliyopo na kutafuta suluhisho la changamoto za jamii. Endapo wahadhiri wataanza kuepuka mijadala ya masuala ya kisiasa, kijamii au kikatiba kwa kuhofia athari zinazoweza kutokea, wanafunzi watanyimwa fursa ya kupata elimu inayowajengea uwezo wa kufikiri kwa kina na kujitegemea. Kwa muda mrefu, hali hiyo inaweza kupunguza ubora wa wahitimu wanaozalishwa na vyuo vikuu jambo litakalohatarisha ustawi wa Taifa.

Tatu, **ukamataji wa wanataaluma unadhoofisha shughuli za utafiti na uchapishaji wa kazi za kisayansi**. Tafiti nyingi za kijamii, sheria, siasa na utawala zinahitaji watafiti kuchunguza masuala yanayohusu sera za umma, utawala na haki za binadamu. Ikiwa watafiti wataona kuwa uchambuzi wa masuala hayo unaweza kuwaweka katika hatari ya kuchunguzwa au kukamatwa, baadhi yao wanaweza kuacha kufanya tafiti katika maeneo hayo. Matokeo yake ni kupungua kwa tafiti zinazoweza kusaidia serikali na jamii kutatua changamoto mbalimbali kwa kutumia ushahidi wa kisayansi.

Nne, **matukio ya ukamataji yanaathiri uhuru wa taasisi za elimu ya juu** (*Institutional Autonomy*). Uhuru wa taaluma hauhusiani na haki za wanataaluma pekee bali pia uwezo wa vyuo vikuu kujiendesha kama taasisi zinazozalisha maarifa. Endapo mazingira yatajengeka kwamba mijadala ya kitaaluma inaweza kuingiliwa na mamlaka za nje, uongozi wa vyuo unaweza kuanza kuweka masharti makali kuhusu mihadhara, semina au tafiti zinazofanyika chuoni ili kuepusha migogoro. Hali hiyo inaweza kupunguza nafasi ya vyuo vikuu kuwa maeneo huru ya mijadala ya kitaaluma.

Tano, **ukamataji wa wanataaluma unaathiri uhusiano kati ya wanafunzi na walimu**. Katika mazingira ya kawaida ya kitaaluma, wanafunzi wanatarajiwa kushiriki mijadala ya wazi na walimu wao kuhusu masuala mbalimbali ya kitaaluma na kijamii.

Hata hivyo, iwapo wanafunzi wataona kuwa kushiriki katika mijadala hiyo itawaweka walimu wao katika hatari ya hatua za kisheria, wanaweza kupunguza ushiriki wao au kuacha kabisa kuuliza maswali kuhusu masuala yanayohusu sera za umma na utawala. Hivyo, mazingira ya kujifunza yanakuwa ya tahadhari badala ya uhuru wa kufikiri.

Sita, **matukio hayo yanaathiri taswira ya vyuo vikuu vya Tanzania katika jumuiya ya kimataifa**. Katika viwango vya kimataifa, uhuru wa taaluma ni mojawapo ya vigezo vinavyozingatiwa katika ushirikiano wa kitaaluma, ufadhili wa tafiti na ubadilishanaji wa wanataaluma. Taasisi nyingi za kimataifa hupendelea kushirikiana na vyuo vikuu vinavyoonekana kuwa na mazingira yanayolinda uhuru wa kufanya utafiti na kutoa maoni ya kitaaluma. Hivyo, matukio yanayoibua wasiwasi kuhusu uhuru wa taaluma yanaweza kuathiri uwezo wa vyuo vikuu vya Tanzania kuvutia ushirikiano wa kimataifa, ruzuku za utafiti na watafiti kutoka nje ya nchi.

Saba, **ukamataji wa wanataaluma utaathiri maendeleo ya demokrasia na utawala bora**. Vyuo vikuu vina jukumu la kuzalisha maarifa yanayosaidia kutathmini sera za umma na kutoa mapendekezo ya maboresho. Wanataaluma wanapochangia mijadala ya kitaifa kwa kutumia ushahidi wa kisayansi, wanasaidia kujenga utamaduni wa uwajibikaji na kufanya maamuzi yanayotegemea ushahidi. Endapo ushiriki huo utapungua kutokana na hofu ya hatua za kisheria, taifa linaweza kupoteza mchango muhimu wa wataalamu katika kutatua changamoto za maendeleo.

Kwa ujumla, athari za ukamataji wa wanataaluma haziishii kwa watu binafsi wanaokamatwa, bali zitaathiri mfumo mzima wa elimu ya juu. Ukamataji utaathiri ufundishaji, utafiti, kujifunza na kushiriki katika mijadala ya kitaaluma. Hivyo, ili vyuo vikuu viendelee kutekeleza wajibu wake wa kuzalisha maarifa, ubunifu na suluhisho la changamoto za Taifa, ni muhimu kuhakikisha kwamba utekelezaji wa sheria unaenda sambamba na ulinzi wa uhuru wa taaluma.

## 6. Hitimisho

Tunahitimisha kwa kuweka bayana kwamba, kulinda uhuru wa taaluma si kwa ajili ya wanataaluma pekee, bali ni kwa ajili ya mustakabali wa Taifa. Vyuo vikuu ndivyo vinavyowalea na kuwaandaa watunga sera, wanasheria, askari, watumishi wa umma,

madaktari, wahandisi na viongozi wa kisiasa. Iwapo mazingira ya elimu yataongozwa na hofu, vitisho au ukandamizaji badala ya uhuru wa kufikiri, kuhoji na kutafuta ukweli kwa misingi ya ushahidi, basi Taifa litazalisha wataalamu wanaoogopa kuuliza maswali magumu, kutoa ushauri huru na kutetea haki pale inapohitajika.

Taifa linalotamani kuwa na mahakama huru, vyombo vya dola vinavyotenda kwa weledi na kwa kuzingatia sheria, utumishi wa umma wenye uadilifu, pamoja na uongozi wa kisiasa unaofanya maamuzi kwa busara na kwa maslahi ya wananchi, haliwezi kupuuza umuhimu wa kulinda uhuru wa taaluma. Wanaotekeleza sheria na kusimamia taasisi za dola nao hufundishwa katika vyuo vikuu; hivyo ubora wa maamuzi yao ya baadaye hutegemea ubora na uhuru wa elimu walioipata.

Kwa hiyo, kulinda uhuru wa taaluma si kulinda maslahi ya kundi la wanataaluma pekee, bali ni kulinda ubora wa taasisi zetu, utawala wa sheria, demokrasia, maendeleo ya kisayansi na uwezo wa taifa kujijenga kupitia maarifa. Elimu huru huzaa fikra huru, na fikra huru hujenga taifa lenye haki, uwajibikaji, ubunifu na maendeleo endelevu.

## 7. Mapendekezo

Kwa kuzingatia athari zinazoweza kujitokeza kutokana na ukamataji wa wanataaluma kwa tuhuma zinazohusiana na shughuli zao za kitaaluma na kwa kuimarisha uhuru wa taaluma katika vyuo vikuu Tanzania , THTU inapendekeza yafuatayo: -

i. Serikali inapaswa kufanya marekebisho ya Sheria ya Vyuo Vikuu ili kutambua kwa uwazi uhuru wa taaluma (academic freedom) kama haki ya msingi katika elimu ya juu. Kwa sasa, ulinzi wa uhuru wa taaluma unatokana zaidi na tafsiri ya haki za kikatiba kama vile uhuru wa kujieleza na kupata taarifa. Kutungwa kwa masharti mahsusi kutatoa mwongozo wa wazi kuhusu haki na wajibu wa wanataaluma pamoja na mipaka ya uhuru huo.
ii. Sheria ya Vyuo Vikuu Na. 7 ya mwaka 2005 inapaswa kufanyiwa marekebisho ili kujumuisha masharti yanayolinda uhuru wa kufundisha, kufanya utafiti, kuchapisha matokeo ya tafiti na kushiriki katika mijadala ya kitaaluma bila kuingiliwa isivyo halali.

iii. Vyombo vya dola vinapaswa kutofautisha kati ya shughuli halali za kitaaluma na vitendo vinavyoweza kujumuisha makosa ya jinai. Maoni yanayotolewa darasani, katika tafiti au mijadala ya kitaaluma yanapaswa kutathminiwa kwa kuzingatia mazingira ya kitaaluma na sio jinai.

iv. Vyuo vikuu vinapaswa kuimarisha uhuru wa taasisi (*Institutional Autonomy*) kwa kuweka sera za ndani zinazolinda uhuru wa wanataaluma katika kufundisha, kufanya utafiti na kutoa maoni ya kitaaluma.

v. Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), Vyama vya wafanyakazi (THTU kikiwemo) pamoja na Jumuiya za wanataaluma, vinapaswa kushirikiana kuandaa miongozo ya kitaifa kuhusu uhuru wa taaluma.

vi. Wanataaluma wanapaswa kuendelea kutekeleza wajibu wao kwa kuzingatia maadili ya taaluma, uadilifu wa kisayansi na matumizi ya ushahidi.

vii. Serikali na uongozi wa vyuo vikuu wanapaswa kujenga utamaduni wa mazungumzo na ushirikishwaji katika kushughulikia migogoro inayojitokeza ndani ya taasisi za elimu ya juu. Ushirikiano huo utasaidia kuondoa utata wa kauli ya **maagizo/maelekezo kutoka juu** ambayo inakuwa kikwazo kikubwa kwenye ufanyaji wa maamuzi ikiwemo utoaji wa dhamana.

viii. Tanzania inapaswa kuendelea kuzingatia na kutekeleza kikamilifu viwango vya kimataifa na kikanda vinavyolinda uhuru wa taaluma, hususan UNESCO Recommendation (1997), Dar es Salaam Declaration (1990) na Kampala Declaration (1990).

Imetolewa na



Paul Loisulie,
Mwenyekiti wa THTU Taifa